

Matumizi salama ya salfa kudhibiti ubwiri kwenye mikoroshu

Tambua tatizo

Ubwiri unga ni ugonjwa wa kuvu unaoshambulia majani machanga, maua na matunda ya koroshu. Ugonjwa huu usipodhibitiwa unaweza kupunguza mavuno kwa zaidi ya asilimia 80.

Vumbi la rangi ya kijivu au jeupe huonekana juu ya majani machanga, maua na matunda yaliyoshambuliwa. Majani yaliyoshambuliwa sana hujikunjakunja na hatimaye huanguka. Maua yaliyoshambuliwa hushindwa kuzaa matunda. Matunda machache yanayozaliwa hudumaa, hupasuka, huoza na huanguka yakiwa machanga.

Habari tangulizi

Ugonjwa wa Ubwiri unga huonekana zaidi wakati wa ukame na hupungua kipindi cha mvua. Vimelea vya ugonjwa huu hujificha kwenye majani ya machipukizi machanga yaliyobanana na huweza kusambazwa kwa njia ya upepo kutoka msimu mmoja hadi mwingine.

Usimamizi

- Ugonjwa huu huweza kudhibitiwa kwa kutumia aina nyingi za kemikali lakini Salfa ya unga hutumika zaidi kwa sababu ina madhara madogo kwa mtumiaji.
- Salfa hupulizwa baada ya kuona asilimia tano ya miti yote ya koroshu imeshambuliwa.
- Salfa hujazwa kwenye tenki la bomba la kupulizia kwa ujazo unaoshauriwa.
- Wakati unaofaa kupulizia ni kuanzia saa 12.00-3.00 asubuhi kwani umande uliopo kwenye majani husaidia Salfa inase.
- Kiwango cha upulizaji ni robo kilo (1/4) kwa mti sawa na kilo 87.5 kwa hekta kwa msimu.
- Kwa msimu, Salfa hupulizwa mara tano (5) kila baada ya siku 14, lakini mpulizo wa mwisho ambao ni wa tano hupulizwa baada ya siku 21.
- Mpulizaji anashauriwa kupulizia Salfa sambamba na upepo unakoelekea ili isimrudie na kumdhuru.

Daraja la 1 la viwatilifu kulingana na shirika la Afya Duniani (WHO) (na bidhaa yenye kibandiko chekundu kwa Tanzania) hazishauriwi kutumika. Daraja la II la viwatilifu kulingana na WHO (na bidhaa yenye kibandiko cha njano-Tanzania), (hazishauriwi Tanzania kutokana na Mpango wa Udhibiti Husishi wa Visumbufu vya Mimea). WHO hupendelea daraja la 3 au U, na Tanzania inashauri bidhaa zenye kibandiko cha kijani au bluu. Kagua na zingatia kutumia Viwatilifu vilivyosajiliwa na (MAFC / TPRI).

Wakati wa kutumia kemikali, vaa mavazi ya kinga wakati wote na ufuate maelekezo kwenye lebo ya bidhaa, kama vile kipimo, majira ya kuweka, muda kabla ya kuvuna

Vumbi jeupe la ugonjwa linavyoonekana kwenye majani. (Picha na apsnet.org)



Vaa nguo ndefu mwili wote kofia na miwani kuzuia sumu isiguse mwili. (Picha na sharp pro)



Jina la kisayansi > *Oidium anacardii*

Mapendekezo katika vidokezo hivi yanatumika katika: Tanzania



WAANDISHI: Costantine P. Mboya, Caroline S. Swai, Jubilant Mwangi
DAEO Mkuranga District Council, Tanzania; Ministry of Agriculture, Food Security
and Cooperatives MAFC- Extension Services FEU
Barua pepe: cosmboya@gmail.com, cswai@yahoo.co.uk

Mwisho na Plantwise